Tangazo la Serikali Na. 552 la tarehe 28/9/2018

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA NA 272)

_____

AGIZO

_____

(Imetolewa kwa kujibu wa Kifungu Na. 28(d))

_____

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI TANGA (“TANGA WSSA”), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga (“Tanga WSSA”), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2018.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Oktoba 2018.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Tanga WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la

Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti ya Tanga WSSA kufanya yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 31 Disemba 2018 au kabla, kuwasilisha EWURA, Mpango wake wa Kibiashara unaojumuisha Mpango wa Uwekezaji utakaozingatia uwekezaji kutokana na fedha zitakazopatikana kutokana na bei mpya kwa kiasi cha Shilingi 4,892.15 milioni mwaka 2018/19 na Shilingi 5,902.55 million mwaka 2019/20. Mpango wa Uwekezaji utatakiwa kuzingatia kufanya uwekezaji katika maeneo yenye miundombinu chakavu ya mabomba ya majisafi na majitaka pamoja na maeneo yanayohitaji kuunganishwa kwa huduma ya majisafi na majitaka kwa mara ya kwanza;

(b) Ifikapo tarehe 31 Disemba 2018 au kabla, kuwasilisha mpango wa utekelezaji wa

masharti ya Agizo hili;

(c) Kuongeza uwezo wa tanki za kuhifadhia maji ifikapo tarehe 30 Juni 2020 kufikia ujazo usiopungua 13,000m^3 kwa siku;

(d) Kuongeza mtandao wa majisafi kufika Kirare na Chongoleani ifikapo tarehe 31 Disemba 2019;

(e) tafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Pili la Agizo hili.

(f) Tanga WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(g) Katika wasilisho lijalo la marekebisho ya bei, mamlaka ya majisafi Tanga itahakikisha madaraja ya bei za maji yanayopendekezwa yanawiana na matakwa ya Kanuni za

Kuwasilisha Maombi ya Kurekebisha bei na tozo;

(h) Tanga WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Tanga WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Tanga WSSA katika siku zijazo.

Kutengua Agizo Gazeti la Serikali Na. 461 la 2014

Agizo hili linatengua Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga ("Tanga WSSA') la kurekebisha bei za huduma ya maji na usafi wa mazingira la mwaka 2014 na mabadiliko yake mengine.

Majedwali

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji Zilizoidhinishwa (Shilingi/ mita ya ujazo)

Kundi la Wateja		Bei ya Sasa	Bei Iliyopendekezwa		Bei Iliyoidhinishwa	
		2017/18	2018/19	2019/20	2018/19	2019/20
Majumbani	0 – 5	1,245	1,711	2,001	1,550	1,710
	>5 – 10	1,315	1,823	2,132	1,635	1,805
	>10 – 30	1,455	2,017	2,359	1,810	1,995
	>30	1,665	2,308	2,699	2,070	2,285
Taasisi	0 – 5	1,245	1,726	2,018	1,550	1,710
	>5 – 10	1,315	1,823	2,132	1,635	1,805
	>10 – 30	1,455	2,017	2,359	1,810	1,995

	>30	1,665	2,308	2,699	2,070	2,285
Biashara	0 – 10	1,525	2,114	2,472	1,900	2,095
	>10 – 30	1,665	2,308	2,699	2,070	2,285
	>30	1,810	2,509	2,935	2,250	2,485
Viwanda	0 – 30	1,595	2,211	2,586	1,985	2,190
	>30	1,950	2,703	3,162	2,425	2,675
Magati		500	693	811	625	690
Mteja mkubwa		1,525	2,211	2,586	1,900	2,095
Wastani wa Bei		1,446	2005	2,345	1,798	1,983

Jedwali Namba 1(b): Bei za Majitaka Zilizoidhinishwa (Shilingi/ mita ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Iliyopendekezwa		Bei Iliyoidhinishwa	
	2017/18	2018/19	2019/20	2018/19	2019/20
Domestic	350	500	550	450	500
Commercial	450	600	650	600	650
Institution	550	800	900	800	900
Industrial	600	850	950	850	950

Jedwali Namba 1(c): Tozo Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya ya Majisafi na Majitaka (Shilingi/Ungaunisho)

<table>
<tr><td rowspan="2">Kundi la Wateja</td><td>Tozo ya Sasa</td><td colspan="2">Tozo Iliyopendekezwa</td><td colspan="2">Bei Iliyoidhinishwa</td></tr>
<tr><td>2017/18</td><td>2018/19</td><td>2019/20</td><td>2018/19</td><td>2019/20</td></tr>
<tr><td>Majumbani</td><td rowspan="4">Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013</td><td colspan="2" rowspan="4">Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013</td><td colspan="2" rowspan="4">Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013</td></tr>
<tr><td>Biashara</td></tr>
<tr><td>Taasisi</td></tr>
<tr><td>Viwanda</td></tr>
</table>

Jedwali Namba 1(d): Tozo Iliyoidhishwa ya Kurejesha Huduma ya Maji (Shilingi/Rudisho la huduma)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyopendekezwa		Bei Iliyoidhinishwa	
	2017/18	2018/19	2019/20	2018/19	2019/20
Majumbani	10,500	10,500	10,500	10,500	10,500

Taasisi	15,000	15,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	15,500	15,500	15,500	15,500	15,500
Viwanda	21,500	21,500	21,500	21,500	21,500

Jedwali Namba 1(e): Tozo iliyoidhinishwa ya Kumwaga Majitaka (Shilingi/Safari)

	Tozo ya Sasa	Tozo Iliyopendekezwa		Tozo Iliyoidhinishwa	
	2017/18	2018/19	2019/20	2018/19	2019/20
Tozo ya kumwaga majitaka	N/A	9,500	10,00	9,500	10,000

JEDWALI LA PILI
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2019/20)

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji	
		2018/19	2019/20
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	No.	2,000	2,000
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	No.	50	50
Kiwango cha Upotevu wa Maji	%	24.2	23.7

Wateja wenye dira	%	100	100
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	95	95

Dodoma
30 Agosti 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu